

# Gazeti

www.ports.go.tz | Bendera Tatu S.L.P. 9184 Dar es Salaam | Email: ccu@ports.go.tz | Namba za Bure: 0800110032 / 0800110047

## KIKAO CHA BARAZA KUU TOENI MAJIBU YENYE KUJITOSHELEZA - KAKOKO



Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Mhandisi Deuseddit Kakoko alipokuwa akifungua Kikao cha 24 cha Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu la Wafanyakazi.

NDANI

BANDARI YA MTWARA  
YAJIDHATITI KUHUDUMIA  
SHEHENA YA KOROSHO

02

KAKOKO AWATAKA  
WADAU WA USAFIRISHAJI  
KUPUNGUZA GHARAMA

04

MV. MBEYA KUTATUA  
CHANGAMOTO ZA  
USAFIRI ZIWA NYASA

10

WAZIRI MPANGO  
AIPONGEZA TPA

12

### Na Innocent Mhando

**M**kurugenzi Mkuu Eng. Deuseddit Kakoko amewaasa Wajumbe kuwasilisha hoja na ushauri kwa usahihi na uwazi ili zijadiliwe kwa pamoja na hatimaye kufanyika maamuzi ya kuipeleka TPA mbele.

Kakoko amewaasa Wakurugenzi wa TPA kuwa makini na hoja za kikao na kutoa taarifa kamilifu, sahihi na za wakati wa sasa ili hatimaye zipokelewe na kujadiliwa na wajumbe kwa maslahi ya TPA na Taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Mkuu ameyasema haya katika Kikao cha 24 cha Kamati ya Utendaji ya Baraza kuu la Wafanyakazi kilichofanyika hivi karibuni.

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Baraza kuu la Wafanyakazi wametakiwa kuzingatia kwamba kikao hicho ni muhimu kwa maslahi ya TPA hivyo

ni vyema mapendekezo yatakayowasilishwa yawe sahihi ili kuleta matokeo chanya katika kushughulikia changamoto mbalimbali.

“Kikao hiki ni muhimu sana pengine kuliko vikao vingine kwa kuwa ndicho kinachotoa ushauri na mapendekezo na hatimaye kuweza kuyatekeleza kwa nia ya kusonga mbele kwa ufanisi,” amebainisha Eng. Kakoko.

# BANDARI YA MTWARA YAJIDHATITI KUHUDUMIA SHEHENA YA KOROSHO, MSIMU WA MWAKA 2018/ 2019

Na Fassie Obadia

**B**andari ya Mtwara imejipanga kuhudumia shehena ya Korosho katika mwaka 2018/2019 ambapo imejiwekea lengo la kuhudumia tani 250,000 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 6.5 ya kiasi cha korosho kilichohudumiwa katika mwaka wa fedha uliopita 2017/2018.

Katika mwaka 2017/2018 jumla ya tani 229,397 za koroshu zisizobanguuliwa zilisafirishwa kupitia Bandari ya Mtwara. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 6.27 ikilinganishwa na tani 215,852 zilizosafirishwa kupitia Bandari hii kwa mwaka 2016/2017.

Kwa mwaka huu meli ya kwanza ya Makasha inatarajiwa kutia nanga katika Bandari ya Mtwara mwanzoni mwa mwezi Oktoba ambapo inatarajia kushusha makasha matupu kwa ajili ya matayarisho ya kusafirishia shehena hiyo ya koroshu.

Mipango ya usafirishaji inafanyika kupitia Kikao cha Wadau wa mnyororo wa usafirishaji wa Koroshu ambacho kinatarajiwa kufanyika mwishoni mwa Septemba, 2018. kikao hicho kitawapa fursa wadau kuelewa jinsi ambavyo Mamlaka imejipanga kuhudumia shehena hiyo ya Koroshu.

Vile vile Mamlaka imejipanga kuhakikisha kwamba changamoto zilizojitokeza mwaka jana zote zinatatuliwa.

Baadhi ya changamoto hizo zilikuwa ni pamoja na ufinyu wa gati usiwezesha meli kubwa zaidi ya moja kuegeshwa kwa wakati mmoja, upungufu wa vifaa vya kupakua au kupakia mizigo kutoka melini kama vile 'Reachstacker', 'Terminal Tractors' pamoja na uchakavu wa vifaa vya kuhudumia mizigo kwenye yadi, kutoweza kuingiza au kuongoa meli wakati wa usiku, ubovu wa maeneo ya kuhifadhia makasha na ubovu wa barabara ya kuingia Bandarini kupitia geti Na. 3.

Kuelekea msimu wa koroshu mwaka 2018/2019 Mamlaka imeiongezea Bandari ya Mtwara vitendea kazi ikiwemo Reach Stacker moja ambayo imeshushwa hivi karibuni bandarini Mtwara.



Changamoto ya ufinyu wa gati itatatuliwa kwa kutumia mita zote 385 za maegesho ya meli na Mamlaka tayari imeanza ujenzi wa gati mpya yenye urefu wa mita 300, upungufu wa vifaa tayari Mamlaka imejipanga kuipatia Bandari ya Mtwara 'Reach Stacker' moja, 'Empty Handler' moja (5) High, na 'Forklift' moja 20Tons ili kuongeza ufanisi.

Kuingiza au kutoa meli usiku changamoto hii inakabiliwa kwa kutengeneza maboya 'Inner Harbour' ili kuwezesha meli zinazomaliza kazi usiku kuhamia 'Inner anchorage' na kuruhusu meli iliyopo 'Inner anchorage' kuingizwa gatini usiku, ubovu wa maeneo ya kuhifadhia makasha Mamlaka inatarajia kufanya 'Paving' mita za mraba 5,600 na ubovu wa barabara geti Na. 3. Tayari Mamlaka imewasiliana na Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani kuhusu ukarabati wa barabara hiyo.

Mikakati kadhaa imewekwa na Bandari kwa lengo la kuboresha utendaji wa Bandari katika msimu huu wa kuhudumia shehena ya koroshu.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutoa huduma kwa saa 24 kwa siku zote 7 za wiki, kuhudumia meli kwa muda usiozidi saa 96, kuwa na vikao vya kupanga shughuli za utendaji wa Bandari (Port Planning Meeting) siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa pamoja na kuendelea kutumia mifumo ya kielektroniki katika kuhudumia meli na mizigo (Harbour View System, Cargo System and Billing System).

Bandari ya Mtwara imekamilisha maboresho makubwa ya miundombinu yake kwa kuongeza yadi za kufanyia 'stuffing' na zile za kuhifadhia makasha matupu. Zaidi ya mita za mraba 38,000 zimeandaliwa kwa ajili ya kufanyia 'stuffing' na mita za mraba 36,000 kwa ajili ya Yadi za kuhifadhia makasha matupu.

Kuendelea kuimarisha ulinzi wa Bandari ya Mtwara na mali za wateja kipindi chote cha msimu wa Koroshu. Uthibiti (access control) wa watu, vyombo vya ausafiri Bandarini sanjari na ukaguzi wa makini wa nyaraka za mizigo ni miongoni kwa mambo yatakayopewa kipaumbele msimu huu.

# HAYAWI HAYAWI SASA...

## • MELI YENYE UREFU WA MITA 220 YATIA NANGA BANDARI YA TANGA

Meli kubwa inayojulikana kwa jina la "Excel Sior" ikiwa imetia nanga katika Bandari ya Tanga ikiwa na shehena ya mafuta ya zaidi ya tani elfu kumi na moja 11 zinazo pelekwa katika nchi jirani ya Zambia hivi karibuni.



Na Moni Jarufu

**K**wa mara ya kwanza Bandari ya Tanga imeweka historia mara baada ya kupokea meli kubwa yenye urefu wa mita 220 iliyobeba shehena ya mafuta na kufanikiwa kutia nanga katika gati la kupokelea mafuta lililopo eneo la Raskazone Jijini Tanga.

Meli hiyo inayojulikana kwa jina la "Excel Sior" imewasili katika Bandari ya Tanga ikiwa na shehena zaidi ya tani elfu kumi na moja za mafuta zinazopelekwa katika nchi jirani ya Zambia ambapo takribani malori 120 yalitumika kusafirisha shehena hiyo kutoka katika bohari kuu ya kampuni ya mafuta ya GBP.

Akizungumza wakati wa kupokea meli hiyo Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Bw. Percival Salama amesema kuwa baada ya kupokea meli hiyo kubwa imedhihirisha sasa Bandari ya Tanga ina uwezo wa kupokea meli yenye ukubwa wa aina yoyote kutokana na kuwa na miundombinu mizuri ya upokeaji meli.

Ameongeza kuwa kuendelea kuwasili kwa meli kubwa katika Bandari ya Tanga pamoja na Jiji la Tanga kwa ujumla kutaongeza fursa za ajira kwa wakazi wa Jiji la Tanga kutokana na

kuwepo na wageni wengi akitaja mfano wa madereva wa malori 120 waliofika tayari wakitokea nchi ya Zambia.

Kaimu Meneja wa Bandari huyo pia amesema kuwa Bandari ya Tanga kwa kuhudumia meli hii kubwa kwa mara ya kwanza katika historia ya Bandari hiyo imeanza kutimiza moja ya mkakati wake wa kuhudumia mzigo wa (transit.) Alisema, "moja ya mkakati wetu tuliojipangia ni kuhudumia "transit cargo" ambapo hapo awali hatukuwahi" kuhudumia.

Katika kufanikisha kupokea meli hiyo Bw. Percival Salama alimshukuru na kumsifu "Harbour Master" wa Mamlaka, Capt. Abdallah Mwingamno kwa kuweza kufanikisha kwa umahiri kutia nanga meli hiyo na kuhudumiwa kwa ufanisi.

Kwa sasa Bandari ya Tanga inahudumia katika nchi jirani shehena mbalimbali za mizigo hususani shehena ya mafuta ambapo nchi za Congo pamoja na Zambia zikiwa ni mojawapo. Kwa kuhudumia nchi jirani Bandari ya Tanga inaongeza mapato sio tu kwa Bandari yenyewe lakini pia kwa Jiji la Tanga na Serikali kwa ujumla.



Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga Bw. Percival Salama (aliyenyoosha mkono) akizungumza jambo wakati wa kupokea meli kubwa yenye urefu wa mita 220 yenye shehena ya mafuta ilipotia nanga katika gati la kupokelea mafuta lililopo Raskazone Jijini Tanga hivi karibuni.



# KAKOKO AWATAKA WADAU WA USAFIRISHAJI KUPUNGUZA GHARAMA ZA KUFANYA BIASHARA



Eng. Deuseddit Kakoko alipokuwa akitoa Mada kwa Wajumbe wa mkutano wa ISCOS (hawapo pichani)

Na Janeth Ruzangi

**M**

kurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deuseddit Kakoko amewataka wadau wa Ushoroba wa Kati (Central Corridor) kutumia fursa zilizopo ili kupunguza gharama za kufanya biashara.

Mhandisi Kakoko ameyasema hayo wakati wa ufunguzi wa warsha ya Kimataifa iliyoandaliwa na Kamati ya Serikali ya Kudumu ya Usafirishaji (Inter

Governmental Standing Committee on Shipping- ISCOS) iliyofanyika Septemba 19-20, 2018 jijini Dar es Salaam.

Kakoko amesema ni jukumu la wadau wa usafirishaji kujipanga vizuri ili kuokoa muda wa safari na kutoa huduma bora katika usafirishaji wa mizigo ya wateja

## Kakoko awataka Wadau wa usafirishaji kupunguza gharama za kufanya biashara

Baadhi ya Wajumbe wakifuatilia Mada iliyokuwa ikitolewa na Eng. Deusdediti Kakoko (Hayuko pichani) hivi karibuni Jijini Dar es Salaam.



kwa kuondoa vikwazo mbalimbali.

Alitoa mfano kuwa, kuna shehena ya tani takriban milioni 40 mpaka 50 katika Ushoroba wa Kati ambayo wadau wanashindwa kutumia fursa kuihudumia, na badala yake ni tani milioni 16.2 tu ambazo zinapita katika

Ushoroba huo.

“Changamoto nyingi zinatokana na wadau kutotumia vizuri fursa zilizopo katika shoroba zetu haswa hii ya Kati katika kupunguza gharama za biashara,” amesema.

Kamati hiyo ambayo imeundwa na nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Zambia imeendesha warsha ya siku mbili ambayo imewakutanisha wadau wa usafirishaji kujadili masuala mbalimbali yatakayohusu usafiri wa majini na nchi kavu kwa kaulimbiu isemayo “International Freight Logistics Best Practices.”

Akizungumzia kuhusu mikakati ya TPA kama lango la biashara nchini, Kakoko amesema asilimia 90 ya biashara ya Kimataifa hapa nchini inapitia katika bandari na hivyo TPA imejipanga kuwekeza katika miundombinu na vifaa vya kisasa, kuendeleza rasilimali watu, kuongeza na kuboresha matumizi ya TEHAMA, kuendeleza juhudi za kimasoko ili kumsogeza mteja karibu na kudumisha usalama wa mizigo katika Bandari zote.

Wakati huohuo Mkurugenzi wa Masoko Bibi Francisca Muindi ametoa mada ya TPA kuhusu jitihada zinazofanyika katika kuboresha huduma zinazotolewa na Bandari ya Dar es Salaam.



*Asilimia 90 ya biashara ya Kimataifa hapa nchini inapitia katika Bandari TPA imejipanga kuwekeza katika miundombinu vifaa vya kisasa, kuendeleza rasilimali watu, kuongeza na kuboresha matumizi ya TEHAMA, kuendeleza juhudi za kimasoko ili kumsogeza mteja karibu na kudumisha usalama wa mizigo katika Bandari zote. Kakoko alisema.*



Wajumbe wakiwa katika picha ya pamoja na Mgeni Rasmi, Katibu Mkuu Dkt. Leonard Chamuriho mwenye dhamana ya Uchukuzi.





## MIDAKI (SCANNERS) YAONGEZEKA BANDARINI

Na Focus Mauki

**M**ahojiano maalumu na Afisa Mkuu anayeshughulikia miradi ya ufungaji wa "Scanners", Bw. Mtani Rugina kuhusiana na hali ya ufungaji wa mashine za kukagulia mizigo kwenye Bandari za mamlaka.

**Swali:** Hali ilikuwaje kabla ya Mamlaka kuanza miradi maalumu ya kujenga na kufunga "scanners" ndani ya Bandari ya Dar es Salaam.

**Jibu:** Kabla ya Mamlaka ya Bandari kujenga na kufunga mashine za midaki (scanners), katika Bandari ya Dar es salaam, ukaguzi wa mizigo iliyowekwa kwenye makasha "Containerized Cargo" ulikuwa unafanyika kupitia midaki michache iliyokuwepo. Midaki hiyo ilikuwa inazidiwa na wingi wa mizigo inayohitajika kukaguliwa hivyo kusasabisha msongamano wa malori ndani ya Bandari jambo ambalo lilikuwa likiisababishia Mamlaka na wadau wake hasara iliyotokana na ucheleweshaji wa mizigo.

**Swali:** Mamlaka imejenga "scanners" ngapi na ni za aina gani ndani ya Bandari ya Dar es Salaam pekee.

**Jibu:** Mamlaka imejenga na kusimika midaki mipya sita (6) katika Bandari ya Dar es Salaam, kati ya hiyo sita (6) midaki mitano (5) imekamilika na kuanza kazi ambapo mitatu (3) ni kutoka kampuni ya Nucotech ya nchini China na miwili (2) ni kutoka kampuni ya AS&E kutoka nchini Marekani. Mdaki wa sita (6) bado upo katika hatua za mwisho za usimikwaji ambao nao umetoka kampuni ya Nucotech ya nchini China.

**Swali:** Je kunatofauti yoyote katika ubora na utendaji wa Scanners za sasa na zamani?

**Jibu:** Midaki iliyojengwa ni ya kisasa zaidi ukilinganisha na iliyokuwepo hapo awali katika nyanja ya uwezo wa ukaguzi wa mizigo kwa saa (throughput), ubora

wa taswira za mizigo ya makasha zinazalishwa na uwezo wa kusoma namba za usajili (registration numbers) wa malori na namba za makasha automatiki. Mathalan, midaki ya "Z Portal and Sentry Co Located Systems" iliyonunuliwa kutoka marekani ina uwezo wa kukagua makasha 240 kwa saa ikilinganishwa na 20-50 kwa saa ya mashine zilizokuwepo awali, midaki hii inatupa taswira za mizigo katika makasha zilizo katika ubora zaidi na hivyo kurahisisha usomaji wa taswira (Radioscopic Image Analysis) na kuongeza ufanisi katika udhibiti wa mapato ya serikali na vitu vilivyozuliwa kuingia au kutoka nchini. Uwezo wa midaki hii kusoma namba za makasha na malori "automatiki" umerahisisha kazi kwa watumishi wanaoendesha hii mitambo na hivyo kuchangia ufanisi katika shughuli za ukaguzi wa mizigo iliyowekwa kwenye makasha "Containerized Cargo".

**Swali:** Ni yapi matumizi (type of cargo scanning) ya kila "scanners" iliyojengwa.

**Jibu:** Midaki iliyokwishasimikwa katika Bandari ya Dar es Salaam inakagua mizigo iliyofungwa kwenye Makasha "Containerized Cargo", hata hivyo Mamlaka iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ununuzi wa midaki itakayokagua aina nyinginezo za mizigo inayopita Bandarini kama vile Magari na Vifurushi.

**Swali:** Je "scanners" zilizopo zinaufanisi wa kiwango gani katika kuhudumia idadi ya mizigo kwa saa.

**Jibu:** Katika Midaki hii mipya iliyosimikwa wa kiwango cha chini una



Lori likipita kwenye Mdaki uliopo Bandari ya Dar es Salaam

uwezo wa kukagua makasha themanini (80) kwa saa na wa kiwango cha juu makasha mia mbili na arobaini (240) kwa saa.

**Swali:** Ni mizigo ya aina gani ambayo itakuwa ikikaguliwa kwenye "scanners".

**Jibu:** Mpango wa Mamlaka uliopo kwa sasa ni kuhakikisha kwamba mizigo ya aina yote inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam inapitishwa kwenye midaki kwa ajili ya ukaguzi. Kutokana na dhamira hii, Mamlaka imejipanga kununua midaki itakayokidhi ukaguzi wa mizigo kutokana na aina ya mizigo husika mathalani midaki inayokagua Mizigo iliyofungwa kwenye Makasha "Containerized Cargo "scanners", midaki itakayo kagua vifurushi vinavyopita eneo la Majahazi (Pallet "scanners") na maeneo mengine.

**Swali:** Ufanisi wa "scanners" upoje kwa maana ya kupunguza msongamano au ucheleweshaji wakati wa kukagua mizigo (scanning process).

**Jibu:** Midaki mipya iliyosimikwa



imepunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la msongamano wa malori uliokuwa unasababishwa na foleni katika maeneo yenye midaki.

**Swali:** Je "scanners" zimenunuliwa kutoka kampuni zipi

**Jibu:** Midaki iliyofungwa imenunuliwa kutoka kampuni mbili kubwa za Nuctech ya China na AS&E kutoka Marekani.

**Swali:** Ni "scanners" zipi ambazo tayari zimekamiliwa.

**Jibu:** Kati ya midaki sita inayosimikwa katika Bandari ya DSM, midaki mitano (5) ndio imeshakamilika na inatumika kwa shughuli za ukaguzi wa mizigo. Midaki iliyokamilika usimikwaji wake ni midaki miwili (2) aina ya "Z Portal & Sentry Co located Systems" na midaki inayohamishika mitatu aina ya MT1213DE.

**Swali:** Je "scanners" ambazo bado hazajakamilika zitakamilika lini.

**Jibu:** Mdaki ambao bado upo kwenye hatua ya usimikwaji ni mdaki wa Reli ya TRL ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi disemba mwaka 2018.

**Swali:** Je Mamlaka ina wataalamu wa kutosha kuendesha na kusimamia "scanners" zilizopo na zinazosimikwa.

**Jibu:** Kwa hakika, Mamlaka inao wataalamu wenye uwezo wa kuendesha na kusimamia shughuli za midaki hii, vilevile Mamlaka ina mipango mbali mbali ya kuwaendeleza wataalamu wake ili wawe wabobezi katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa midaki hii.

**Swali:** Je ujenzi wa "scanners" umezingatia suala la uhifadhi wa mazingira.

**Jibu:** Hakika, usalama wa mazingira na watumiaji wa midaki hii ndani ya Bandari kwa ujumla ni kipaumbele katika usimikwaji na uendeshaji wa midaki hii. Katika kudhibitisha hili, Mamlaka ya Nguvu za Kiatomiki

imeruhusu matumizi ya midaki hii kwa kuwa ni salama kwa mazingira na watumiaji wake.

**Swali:** Je Mamlaka imejenga "scanners" hizo kwa fedha zake.

**Jibu:** Mamlaka imenunua na kujenga Midaki yote sita (6) kwa mapato yake ya ndani.

**Swali:** Kampuni zilizojenga "scanners" zinatambulika Kimataifa?

**Jibu:** Kampuni ya Nuctech Kutoka China na AS&E kutoka Marekani zilizojenga midaki hii ni miongoni ya kampuni kubwa tatu (3) kati ya Makampuni yanayojihusisha na utengenezaji wa mashine za midaki duniani.

**Swali:** Mamlaka imejenga "scanners" katika Bandari nyingine?

**Jibu:** Ndio, Mamlaka imesimika midaki katika Bandari za Tanga na Mtwara. Kuna midaki miwili (2) katika Bandari ya Tanga na Mmoja upo katika Bandari ya Mtwara.

**Swali:** Je "scanners" zilizojengwa zinatoshleza mahitaji ya Bandari zetu?

**Jibu:** Hakika, Midaki iliyojengwa na inayoendelea kujengwa kwa sasa itatosheleza mahitaji ya ukaguzi wa mizigo ya aina mbalimbali katika Bandari ya Dar es Salaam. Mamlaka imekamiliwa ununuzi na usimikwaji wa midaki sita (6) ya ukaguzi wa Mizigo iliyowekwa kwenye makasha "Containerized Cargo" na iko katika mchakato wa ununuzi wa midaki itakayotumika katika ukaguzi wa Magari mara baada ya kukamilika kwa gati la magari "RORO" midaki ya ukaguzi wa vifurushi vya mizigo "Pallets" pale majahazi na ununuzi wa midaki itakayoongezwa katika majengo yote ya kuingia au kutokea Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa sasa haina midaki ya aina hiyo mathalani katika eneo la Azam Sealink.



Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Mhandisi Deuseddit Kakoko, alipokuwa akifunga Kikao cha 24 cha Baraza Kuu la Wafanyakazi.



Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Baraza Kuu la Wafanyakazi wakifuatilia Mkutano wa 24 wa Kamati.



Mjumbe akichangia Mada

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Prof. Ignas Rubaratuka akikagua mchoro wa Mradi Bandarini Mtwara.



Mjukuu wa Malkia wa Uingereza Prince shughuli za Bandari.





Wajumbe wakichangia Mada katika Mkutano wa 24 wa Baraza Kuu.



katika Mkutano wa 24.



Kamati ya Utekelezaji ya Bodi ya Wakurugenzi walipotembelea miradi katika Bandari ya Mtwara.

Mjukuu wa Malkia wa Uingereza Prince William ametembelea Bandari ya Dar Es Salaam na kufurahia utendaji kazi wake. Pichani Mhandisi Deusdedit Kakoko akimkabidhi kinyago cha Twiga kama alama ya Taifa kwa kumbukumbu yake. Kushoto ni Waziri wa Sheria na Katiba Prof. Palamagamba Kabudi akishuhudia.



e William akipata maelezo kuhusu







# MV. MBEYA KUTATUA CHANGAMOTO ZA USAFIRI ZIWA NYASA

Na Leonard Magomba

**K**ukamilika kwa ujenzi wa meli mpya ya abiria ya MV. Mbeya II kunatarajiwa kutatua changamoto za usafiri wa abiria na mizigo katika mwambao wa Ziwa Nyasa.

Meli hiyo ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 80, itakuwa ni meli ya kwanza ya kisasa ya abiria ambayo itaunganisha mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma pamoja na nchi jirani za Malawi na Zambia.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Bw. Abed Gallus amesema kwamba ujenzi wa meli hizo ambao unafanywa na kampuni ya Kizalendo ya Songoro Marine, ni moja ya juhudi zinazofanywa na TPA kuboresha shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo majini.

“Ujenzi wa meli hii ya abiria, ni sehemu ya utekelezaji wa ujenzi wa meli tatu za TPA katika Ziwa Nyasa zilizolenga kutatua changamoto za usafiri wa abiria na mizigo majini,” amesema Gallus.

Bw. Gallus amesema kwamba TPA, ilianzisha mradi wa meli tatu zikiwemo mbili za mizigo zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja na moja ya abiria

yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200.

Amesema kwamba miradi hiyo ilitekelezwa kwa awamu mbili tofauti ambapo awamu ya kwanza ilihusisha meli mbili za mizigo, MV Ruvuma na MV Njombe ambazo ujenzi wake ulikamilika mwezi Julai, 2017.



Ujenzi wa meli ya abiria ya MV Mbeya II ambao umefikia asilimia 80 unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2018 na utagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 9.

Asilimia 20 iliyobaki katika kukamilisha mradi huo wa meli inahusu ufungaji wa engine, generator, uwekaji wa vyumba na mambo mengine madogo madogo katika umaliziaji wa ndani na nje ya meli.

Meli hiyo ya abiria inatarajiwa kuwa kivutio kikubwa sana kwa watumiaji wa usafiri wa majini kutokana na ukweli kwamba itakuwa na uwezo wa kubeba mizigo na abiria kwa wakati mmoja.


MV Mbeya II inatarajia kufanya safari zake katika Bandari mbalimbali kongwe na nyingine mpya zitakazoanzishwa na TPA katika mwambao wa Ziwa Nyasa ili kuleta ufanisi katika usafirishaji wa abiria na mizigo ziwani.

“

*Ujenzi wa meli hii ya abiria, ni sehemu ya utekelezaji wa ujenzi wa meli tatu za TPA katika Ziwa Nyasa zilizolenga kutatua changamoto za usafiri wa abiria na mizigo majini, amesema Gallus.*

”





## WATEJA - WADAU WACHANGAMKIA HUDUMA YA "LIVE CHAT" KATIKA TOVUTI YA TPA

Na Focus Mauki

**W**ateja na wadau mbalimbali wa Mamlaka wameonesha kuchangamkia huduma ya "Live Chat" ambayo inapatikana kwenye dirisha la "Talk to Us" ambayo inapatikana katika tovuti ya Mamlaka kupitia katika kiocha cha [www.ports.go.tz](http://www.ports.go.tz)

Huduma hiyo ambayo inapatikana katika tovuti iliyofanyiwa marekebisho makubwa na idara ya TEHAMA inapatikana kote ulimwenguni, ambapo takwimu zinaonesha watembeleaji (visitors) huingia na kutumia huduma hiyo.

Mbali na huduma hii watembeleaji wengi wameonesha kupitia huduma na maelezo mbalimbali yanayopatikana katika tovuti hiyo wakiwa na malengo ya kupata taarifa au kuuliza maswali kupitia "Live Chat".

Maswali mengi yanayoulizwa na Wateja kupitia huduma hii ni pamoja na taratibu za uingizaji na uondoshaji wa mizigo Bandarini, mawasiliano na wadau wa Bandari pamoja na huduma zinazotolewa na Wadau wengine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Maboresho ya tovuti ya Mamlaka


yamekuja mara baada ya tovuti ya awali kukosa baadhi ya huduma ambazo zingeweka Mamlaka karibu zaidi na Wateja na Wadau wake kwa ujumla.

Hadi kufikia Septemba 07, 2018 kurasa za tovuti ya Mamlaka ambazo zimetembelewa na wasomaji mpaka sasa na takwimu zake katika mabano ni pamoja na ukurasa wa mbele (1,119,143), Dar es Salaam and Central

Coast Sea Ports (18,899), Management (17,093), Overview (16,020) na Cargo Service (14,688).

Mbali na kuwa na tovuti Mamlaka pia inasimamia na kuendesha mitandao ya kijamii ya Facebook, Twitter na Instagram ambayo inapatikana kupitia @tanzaniaportshq.

Kwa upande wa YouTube, taratibu za kupata leseni Online TV kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaendelea na mara itakapo patikana tutaweka vipindi vya TPA lengo likiwa ni kuwafikia watu wengi zaidi.





Kaimu Mkuu wa Bandari ya Mtwara Bw. Abdilah Salim akiwa anatoa maelezo kwa Mh. Waziri wa Fedha Dk. Philip Mpango (kushoto) juu ya miundo mbinu ya kupokela mafuta Bandarini Mtwara

# Waziri Mpango aipongeza TPA

Na Fassie Obadia

**M**amlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imepongezwa kwa jitihada inazofanya za kuendeleza Bandari ya Mtwara kwa kuongeza vitendea kazi pamoja na upanuzi wa gati unaoendelea.

Pongezi hizo zimetolewa na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dk. Philip Mpango wakati alipotembelea Bandari ya Mtwara kukagua miundombinu ya kupokelea mafuta (manfold).

Akiwa Bandarini hapo Waziri Mpango alipokelewa na Kaimu Mkuu wa Bandari ya Mtwara, Bw. Abdilah Salim na Menejimenti ya Bandari ya Mtwara na kupatiwa ufafanuzi wa changamoto mbalimbali zilizojitokeza msimu uliopita wa usafirishaji korosho ikiwemo uhaba wa vitendea kazi, miundombinu na maeneo ya kufanyia kazi.

Dk. Mpango alipewa taarifa kwamba tayari Mamlaka imeshaanza kutatua

changamoto mbalimbali zilizojitokeza msimu uliopita ikiwemo uhaba wa vifaa kwa kuongeza vitendea kazi mbalimbali ambapo hivi karibuni Bandari ya Mtwara inatarajia kupokea vifaa mbalimbali vikiwemo 'Reach Stacker' 2 na 'Terminal Tractor' 6 ambavyo vinatarajiwa kufika kabla ya msimu kuanza.

Vilevile changamoto ya maeneo imeshatataliwa kwa kuendelea kutumia maeneo yaliyoachwa na kampuni ya BG. Mamlaka pia inafanya utaratibu wa kuboresha maeneo ya kuhifadhia makasha kwa kujenga 'Heavy Duty Pavement' katika eneo la 'Casing Yard' kwa ajili ya kuhifadhia Makasha.

Kuhusu Miundombinu na barabara tayari Mamlaka imeweka kwenye bajeti yake ya 2018/2019 mpango wa ukarabati barabara inayotumika kupeleka mizigo 'Dhow wharf' na maeneo mengine yataendelea kufanyiwa ukarabati kadri itakavyowezekana.

Waziri wa Fedha na Mipango aliipongeza Mamlaka kwa kufanya kazi kwa bidii na kuweza kuingizia Serikali mapato kupitia tozo za Bandari na Forodha.

Vile vile aliishukuru Mamlaka kwa kuweza kushirikiana na TRA na kufanya vizuri kwenye msimu wa mwaka uliopita ambao umeingizia Serikali mapato makubwa.



*Akiwa Bandarini hapo Waziri Mpango alipokelewa na Kaimu Mkuu wa Bandari ya Mtwara, Bw. Abdilah Salim na Menejimenti ya Bandari ya Mtwara na kupatiwa ufafanuzi wa changamoto mbalimbali zilizojitokeza msimu uliopita wa usafirishaji korosho ikiwemo uhaba wa vitendea kazi, miundombinu na maeneo ya kufanyia kazi.*







**DAINESS B. JOHN**  
UTEKELEZAJI



**DAMIAN PETER**  
UTEKELEZAJI



**JAFARI MSOKA**  
UTEKELEZAJI



**LUCY MAYAO**  
UTEKELEZAJI



**PRISCA MAGANGA**  
UTEKELEZAJI



**RAYMOND MSUYA**  
UTEKELEZAJI



**SADIKIEL MAKONO**  
UTEKELEZAJI



**SALAMA JENGO**  
UTEKELEZAJI



**USSI MASUDI**  
UTEKELEZAJI



**VERDIAN K. KAGASHANI**  
UTEKELEZAJI



**VICTOR MKOBA**  
UTEKELEZAJI

# MWINYI: CHUKUENI TAHADHARI NA UGONJWA WA SHINIKIZO LA JUU LA DAMU

Na Peter Millanzi

**M**ganga Mfawidhi wa Bandari ya Dar es Salaam, Dr. Abdallah Mwinyi amewataka wafanyakazi wa Bandari kuchukua tahadhari na ugonjwa wa Shinikizo la juu la damu (HTN) au presha ya juu ya damu (pia huitwa shinikizo la mishipa ya damu, HBP).

Mwinyi alisema hayo wakati alipoongea na mwandishi wa habari ofisini kwake hivi karibuni. Alisema huu ni ugonjwa sugu ambapo nguvu ya msukumo wa damu katika mishipa ni kubwa kuliko kawaida na ongezeko hilo husababisha moyo kufanya kazi kupita kiasi ili uzungushe damu katika mishipa ya damu. Kwa kawaida shinikizo la juu la damu halina dalili, ila likidumu lina madhara makubwa kwa afya.

Pia alisema "Shinikizo la juu la damu ndilo sababu kubwa (kiharishi) ya, upoozaji (kiharusi), mshtuko wa moyo (mashambulizi ya moyo), moyo kushindwa kufanya kazi, kutuna kwa ukuta wa moyo na mishipa damu (k.m., kutuna kwa ukuta wa aota au mkole) na chujio la mshipa wa kupeleka damu kwenye moyo".

Ugonjwa huu husababisha ugonjwa sugu wa figo na hata ongezeko la wastani la shinikizo la damu hupunguza matarajio ya muda wa kuishi.


Mwinyi alitanabaisha kwamba, Kuna vipimo viwili vya shinikizo la damu, yaani systolic na diastolic, shinikizo au presha ya systolic ni kipimo cha damu ambacho kinapima nguvu ya msukumo wa damu katika mishipa ya damu wakati moyo unadunda. Shinikizo au presha ya diastole inapima nguvu ya msukumo wa damu katika mishipa ya damu wakati moyo umetulia au kati ya

mapigo ya moyo (diastole).

Kipimo cha kawaida cha shinikizo la damu ni 100–140 milimita za zebaki (mmHg) upande wa systolic (kipimo

damu: shinikizo la juu la damu la asili na shinikizo la damu linalosababishwa na magonjwa mengine. Kadiri ya asilimia 90–95 za watu wanaathiriwa na "shinikizo la juu la damu la asili", yaani wana ugonjwa huu bila kuwa na chanzo cha kisayansi kinachofahamika.

Aidha, magonjwa mengine ya mafigo,



cha juu) na 60–90 milimita za zebaki upande wa diastolic (kipimo cha chini). Shinikizo la juu la damu hutokea kama kipimo kikiwa zaidi ya 140/90 mmHg kwa muda mfrefu.

Kuna aina mbili za shinikizo la juu la

mishipa, moyo, mfumo wa homoni huathiri asilimia 5–10 iliyobaki ya watu wenye shinikizo la damu (ndilo shinikizo la damu linalosababishwa na magonjwa mengine).

Mwinyi ametoa rai kwa Wafanyakazi, ili kudhibiti shinikizo la damu, lishe



bora na mabadiliko katika mtindo wa kuishi lazima yazingatiwe pamoja na kupunguza matatizo yanayoathiri afya. Hata hivyo, matumizi ya dawa ni muhimu kwa watu ambao mabadiliko ya mtindo wa maisha hautoshelezi kupunguza shinikizo la juu la damu, kutuna kwa ukuta wa ateri mithili ya puto kutokana na udhaifu wa sehemu hiyo.

Mwinyi alisema, kwa watu wenye umri wa miaka 18 au zaidi, shinikizo la juu la damu linaweza kuwa systolic na/au diastolic kama kipimo hicho



ni zaidi kuliko kipimo cha kawaida kinachokubalika ambacho ni (139 mmHg systolic, 89 mmHg diastolic: tazama table — Uainishaji (JNC7)).

Kama vipimo vinapatikana baada ya kutumia chombo kinachopima presha

kwa masaa 24 (24-hour ambulatory) au kufanya maangalizi nyumbani, vipimo vya chini vinatumiwa (135 mmHg systolic or 85 mmHg diastolic).

Pia miongozo ya kimataifa ya hivi karibuni imegawanya shinikizo la damu katika vikundi mbali mbali vyenye vipimo chini ya kipimo cha shinikizo la juu la damu ili kuthibitisha hatari iliyopo ya shinikizo la juu la damu.

Aidha Mwinyi alisema, sio kawaida kwa watoto wachanga kuwa na shinikizo la juu la damu ni asilimia 0.2 hadi 3% ya watoto wachanga ambao wanapata. Shinikizo la damu haipimwi mara kwa mara kama watoto ni wadogo na wana afya nzuri.

Pia alisema, watoto na vijana kupata shinikizo la damu (asilimia 2–9% hutegemea na umri, jinsia, na asili) hivyo ni vyema nao wakachunguzwa afya zao na shindikizo la damu. Shindikizo la damu kwa watoto wakati mwingine husababishwa na magonjwa ya figo, moyo na endocrine.

Mwinyi alitanabaisha kuwa, mara nyingi watu wenye shinikizo la damu hawana dalili yoyote, na huwa inagundulika baada ya kufanya uchunguzi kwa kawaida kupitia screening, au wakati maangalizi ya afya yanafanywa kwa sababu nyingine.

Pia, watu wengine wenye shinikizo la damu huwa wanapata, maumivu ya kichwa (haswa nyuma ya kichwa na asubuhi), pamoja na kuchanganyikiwa, kizunguzungu, sikio kelele (mvumo au mazomeo masikioni), kutoweza kuona vizuri au matukio ya kuzirai.

Mwinyi alisema kupima shindikizo la damu kwa mashine maalum BP machine

(sphygmomanometer) hutumika kwa utambuzi. Vipimo vingine vinavyoweza kutumika ni blood urea nitrogen (BUN), creatinine, Serum sodiamu, potasiamu, calcium, thyroid-stimulating hormone, HDL na LDL cholesterol, triglycerides, radiograph kifua, electrocardiogram.

Aidha Mwinyi alisema, dalili zingine zinaweza kusababishwa na magonjwa mengine, yani shinikizo la damu linaloletwa na sababu zingine zinazojulikana kama vile magonjwa ya figo au mabadiliko ya mfumo wa homoni. Kwa mfano, unene wa kifua na tumbo, uthibiti mbaya wa sukari, moon facies au mkusanyiko wa mafuta usoni, mkusanyiko wa mafuta mgongoni ("buffalo hump") na purple striae au alama za unene huonyesha dalili ya ugonjwa wa homoni wa Cushing's syndrome.

Alisema, dalili nyingine, ugonjwa unaoathiri kikoromeo na acromegaly yaani mwili hutengeneza homoni ya kukuza umbo pia huweza kuleta shinikizo la juu la damu na dalili zake za kawaida huonekana Wembamba wa mishipa ya tumbo au abdominal bruit inaweza kuwa ni ishara ya renal artery stenosis au kuziba kwa mishipa ya damu ipelekayo damu kwenye figo Aortic coarctation (kupungua kwa upana wa mshipa mkuu utoao damu kwenye moyo kwenda mwilini).

Pia Mwinyi alisema, shinikizo la damu ambalo linalotofautiana sana na kuumwa kwa kichwa, mpapatiko wa moyo, kubadilika rangi ya ngozi, na utoaji jasho ni lazima kuwe na wasiwasi wa pheochromocytoma yaani saratani ya tezi iliyo juu ya figo.

**Makala hii itaendelea katika toleo lijalo...**

# MATUMIZI "MAKUBWA" YA CHUMVI KWENYE CHAKULA HUSABABISHA KIFO

**M**oyo ni kiungo muhimu sana kwa afya ya mwanadamu. Kazi kubwa ya Moyo ni kusafirisha damu safi kwenda kwenye ubongo na pia kwenye sehemu mbalimbali za mwilini.

Damu pia husafirisha virutubisho mbalimbali mwilini kama chakula na homoni. Vilevile Moyo husukuma damu chafu (isiyo na oxygeni) kwenda kwenye mapafu kwa ajili ya kupata hewa safi.

Sasa basi utaona ni kwa jinsi gani Moyo ni kiungo muhimu sana na ni lazima kitunzwe ili kuweza kufanya kazi vizuri.

Kufanya kazi vizuri kwa Moyo kunaimarisha ufanyaji kazi mzuri wa viungo vingine vya mwili kwa mfano Ubongo, Maini, Figo Mfumo wa usagaji wa chakula. Kwahiyo utaona kuwa Moyo usipofanya kazi vizuri basi kuna hatari ya viungo vyote vya mwili kutofanya kazi vizuri.

Njia nyingi za kuufanya Moyo ufanye kazi vizuri zimefahamika kwa muda mrefu na baadhi ya watu wengi wanazingatia.

Mfano ni kufanya mazoezi ambayo ili yalete tija yanatakiwa kufanywa kwa mfululizo kwa dakika zisizopungua 30 angalau mara nne kwa wiki.

Mazoezi hayo yanaweza kuwa ni kutembea tu. Njia nyingine ni kula vyakula ambavyo havina mafuta na hapa tunasisitiza mafuta ya Wanyama ambayo yana rehemu nyingi, vilevile kupunguza nyama nyekundu.

Vyakula vya mboga mboga nyingi ndivyo hasa yana vime sisitizwa, pia vyakula vya asili ya samaki ni vizuri kwa afya ya Moyo, Vilevile kuto kuvuta sigara.

Sasa watu wengi wamekuwa wakielewa

baadhi ya vyakula tajwa hapo juu kuwa na madhara, sasa wanasayansi wakawa wanajiuliza mbona wale watu ambao hawali kabisa nyama wala mafuta ya Wanyama mbona wanapata magonjwa ya moyo.? Sasa hapo ndio suala la ulaji wa chumvi katika vyakula tunavyokula.

## Chumvi inaua:

Chumvi imethibitika kuwa ni kihatarishi kikubwa ambacho sasa ni dhahiri kwakuwa watu ambao hawali vyakula vyenye mafuta mengi, hawali nyama, wanafanya mazoezi na kuzingatia ulaji mzuri lakini bado wanapata magonjwa ya moyo. Watu hawa wamethibitika kutumia chumvi katika vyakula vyao na wakati mwingine kuongeza chumvi mezani.

Watu wengi pia hutumia chumvi nyingi kukolezea kwenye mboga au kachumbari. Pia kuongeza wakiwa mezani wakila chips, mtu kila kipande cha chips anagusa chumvi, au kila

kifinyango cha nyama anagusa chumvi. Hii ni hatari mno kwa afya bora ya moyo.

Pamoja na kuleta madhara ya shinikizo la damu, kuongeza uwezekano wa kupata kiharusi, magonjwa ya kudhoofisha mifupa, magonjwa ya figo chumvi pia inasababisha kuleta madhara ya unene kupita kiasi, kupata magonjwa ya kupoteza kumbukumbu yaani "Alzheimer".

Utaona kuwa chumvi nyingi katika vyakula ni hatari mno kwa afya zetu.

## Nini Cha kufanya:

Kupunguza au kuacha kabisa kutumia chumvi ya ziada hasa baada ya chakula kupikwa yaani "table salt"

Vyakula vyenye chumvi nyingi kwa mfano vyakula vinavyokaushwa au kuhifadhiwa kwa chumvi nyingi mfano samaki na butter au nyama za porini.

Chumvi itumike kidogo kwa ladha tu na sio vinginevyo.



*"Njia nyingi za kuufanya Moyo ufanye kazi vizuri zimefahamika kwa muda mrefu na baadhi ya watu wengi wanazingatia. Mfano ni kufanya mazoezi ambayo ili yalete tija yanatakiwa kufanywa kwa mfululizo kwa dakika zisizopungua 30 angalau mara nne kwa wiki."*